**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**

**SHULE YA SEKONDARI SANYA JUU**

**S.L.P 84, SANYA JUU-SIHA**

Kumb. Na. SJS/JI/2021/01
Jina la mwanafunzi..........................................................................................

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SANYA JUU, WILAYA YA SIHA, MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021**

## 1.0.UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Sanya Juu Mwaka 2021. Shule ipo umbali wa kilometa mbili (2) kutoka mji wa Sanya Juu.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021 saa 1.15 Asubuhi.

## 2.0.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1.Sareza shule

a) Wavulana watashona suruali mbili (2) za kitambaa cha rangi ya **UGORO** zenye rinda mbili mbele, mifuko mitatu (3), upana wa chini usiwe pungufu ya inchi (16) na sweta rangi ya **UGORO**

b) Wasichana watashona sketi za marinda kumi na mbili (12) (sita mbele na sita nyuma) ambazo zitatakiwa kuvuka chini ya magoti kiasi cha urefu wa inchi 6 na sweta rangi ya **UGORO**

c) Wavulana watavaa shati nyeupe za mikono mifupi mbili (2), soksi nyeusi na viatu vyeusi vya ngozi vya kamba ambavyo sio mabuti.

d) Wasichana watavaa shati nyeupe za mikono mifupi mbili (2), soksi nyeupe ndefu sisizovuka magoti pea 2 na viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu, pia nilazima viwe vya kufunga kwa kamba.

e) Wale wanao vaa hijabu wavae sketi ndefu, shati na hijabu nyeupe.

f) Sare za michezo kwa shule hii ni bukta/track suit na T-shirt ya rangi ya **BLUU** na raba.

Scanned by CamScanner

**2.2.Mahitaji ya darasani**

Madaftari 12 counter books quire 2/3, daftari ndogo 12 kwa ajili ya majaribio ya kila wiki, mkebe wa hesabu (Mathematical set), kalamu za kutosha, penseli, rula na mfutio.

**2.3.Vifaa vya usafi**

Kila mwanafunzi atatakiwa kutunza vifaa vya usafi na kuvirudisha alikovitoa mara baada ya matumizi ili kuepuka upotevu unaoweza kutokea.

**2.4.Huduma ya chakula**

Chakula cha mwanafunzi ni jukumu la mzazi. Wazazi wakiongozwa na kamati yao wataratibu namna ambavyo wanafunzi watapata chakula hapa shuleni. Aidha jambo hili litajadiliwa kwenye kikao cha wazazi kwa tarehe mtakayojulishwa kabla ya masomo kuanza.

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na chombo cha kulia chakula.

**3.0. Sheria na kanuni za shule hii**

3.1. Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya RAIS-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla nijambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (prepration ) wawapo nyumbani baada ya muda wa shule.
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na utakazopewa,
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii,
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule,
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa,
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na
ix. Kutunza mali za shule.

3.2.Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika

Scanned by CamScanner

e) Kupigana au kupiga

f) Kuharibu kwa makusudi mali za shule

g) Kudharau Bendera yaTaifa

h) Kuwa mjamzito/kupata mimba au kusababisha.

i) Kuoa au kuolewa

j) Kutoa mimba

k) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

l) Kukataa adhabu kwa makusudi

m) Kuwa na simu

n) Utoro na kujificha vichakani wakati wa masomo

4.0.Mambo mengine yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hosipitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatolewayo na shule au uongozi unaosimamia shule.

5.0.Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA**

..................................................................

***ELIETA T. KAAYA***

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SANYAJUU SEKONDARI

Scanned by CamScanner

## TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi ………………………………………………………umri……………………

Jina la baba…………………………Kata……………………kijiji………………kitongoji…………

Tarafa……………………Wilaya………………..Namba ya simu ya mzazi/mlezi…………………

S.L.P……………………………………….

Nani anakulipia mchango wa chakula cha mchana (mzazi/ mlezi)……………………………………..

Kama ni mlezi jina……………………………kata…………………..kitongoji………………………

Tarafa………………………Wilaya…………………………….namba ya simu……………………..

S.L.P………………………………………

**Tamko la Mwanafunzi**

Mimi (Mwanafuzi) ……………………………………………………………………nimesoma na kuyaelewa maagizo, maelekezo, sheria na kanuni za kujiunga na shule ya Sekondari SanyaJuu. Pia nakiri kwamba nitafuata sheria na kanuni zote za shule.

**Tamko la mzazi/mlezi**

Mimi …………………………………………………… ambaye ni Mzazi/mlezi wamwanafunzi…………………………………………Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yaliyopo katika fomu hii. Pia nakiri kwamba nitamlipia mwanafunzi tajwa mchango wa chakula cha wanafunzi shuleni. Nakubali kuwa niwajibishwe kwa ukiukwaji wamaelekezo yoyote halali yatakayo athiri uendeshaji wa shughuli za shule.

Sahihi …………………tarehe……………

**NB:** ***Mwanao anapaswa kujaza fomu ya matibabu iliyo ambatishwa na maelezo haya na kuiwasilisha shuleni siku hiyo ya kuripoti.***

Scanned by CamScanner

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**

**SHULE YA SEKONDARI SANYA JUU S.L.P 84, SANYA JUU-SIHA**

TAMKO LA KUKUBALI SHERIA ZA SHULE

(Ijazwe kasha irudishwe shuleni siku ya kuripoti)

JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………………………………..

TAREHE YA KUZALIWA……………………………………………………………………

JINA LA MZAZI/MLEZI……………………………………………………………………

UHUSIANO NA MZAZI/MLEZI……………………………………………………………

**KIAPO CHA UTHIBITISHO**; Mimi ………………………………………, Nikiwa mwanafunzi wa shule hii nakubali kuwa, Umma wa nchi hii, Tanzania ndio ulionipa nafasi hii maalumu ya masomo ya sekondari niweze kutumikia nchi hii katika maendeleo yake. Hivyo basi naahidi kwamba nitajibidiisha hapa shuleni na pia nimalizapo shule, ili kutimiza shabaha hiyo.

Ninakubalina ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe nitatii sheria za shule na amri zote nitakazopewa na walimu wangu. Nikiwa na malalamiko au Maoni niyaonayo nitayafikisha kwa viongozi wa shule kufuatana na utaratibu uliowekwa bila kuogopa chochote.

Tarehe……………………………….. Saini ya mwanafunzi…………..………………

**TAMKO LA MZAZI/MLEZI**

Mimi……………………………………………….nikiwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……………………………………………………naahidi kutimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wamtoto huyu.

Tarehe ………………………………… Saini ya mzazi/mlezi……………………………………

Namba ya Simu…………………………………

Scanned by CamScanner

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
SIHA DISTRICT COUNCIL

## *REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION*

To be completed by a medical officerin a Government Hospitalto all new extracts to Sanya Juu Secondary School.

### P ART A: TO THE MEDICAL OFFICER

..............................................................................

STUDENT FORM NAME: ..........................................................................................

Please examine the above named person who has been selected to join this school for his fitness as a student.

Signature............................................ Designation....HEADMASTER.........................

Name of head of school SANYA JUU S.S.......... Official stamp.................................

MKUU WA SHULE
SANYAJUU SEKONDARI

### P ART B: TO BE COMPLETE BY MEDICAL OFFICER

Blood corny (red and white)...........................................................................................

Stool examination............................................ T.B. test........... ..................................

Eye test........................................................... Ears............ .......................................

Chest.............................................................. Spleen......... .......................................

Abdomen..........................................................................................................................

Pregnancy (girls only)................................................................. ..................................

ADDITION INFORMATION (e.g. physical defeat or impairments)

.............................................................................................................. ..................................

........................................................................................................................................................

Please certify that the above is fit to be admitted/ taken care in secondary school. Kind of care

........................................................................................................................................................

### P ART C: M EDICAL OFFICER CERTIFICATE

I have examined the above named person and consider that *he/she* is not physically fit joining secondary education.

Doctor's name.............................................. Signature........... ........................................

Station........................................................ Date........... ................................................

..............................................

**Official stamp**

Scanned by CamScanner